



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
TANGAZO LA KUJIUNGA NA VITUO ATAMIZI VYA UNENEPESHAJI NG'OMBE WA
NYAMA KIBIASHARA KWA VIJANA

1. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Taasisi zake za Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (**TALIRI**) inakaribisha maombi ya kujiunga na **Vituo Atamizi** vya unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama kibiashara katika vituo vifuatavyo: **LITA Buhuri (Tanga), LITA-Mabuki (Mwanza), LITA-Kikulula (Kagera), TALIRI-Mabuki (Mwanza) na TALIRI-Tanga (Tanga).**
2. Washiriki watalelewa katika Vituo Atamizi kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.
3. Sifa za muombaji:-
 - i. Awe raia wa Tanzania;
 - ii. Awe mhitimu wa mafunzo ya mifugo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada au Shahada kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali; na
 - iii. Awe na umri kati ya miaka 18-30.
4. Fomu ya kujiunga na Vituo hivi inapatikana kupitia tovuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ni www.mifugouvuvi.go.tz au www.lita.go.tz au www.taliri.go.tz. Fomu ya maombi iambatishwe na nakala za vyeti vya masomo vilivyothibitishwa, kivuli cha kitambulisho cha NIDA cha muombaji na kivuli cha kitambulisho cha NIDA cha mdhamini. Fomu hiyo na viambatisho vitumwe kupitia barua pepe lita.hq@lita.go.tz au hq@taliri.go.tz
5. Waombaji watakoachaguliwa katika hatua ya kwanza wataitwa kwa ajili ya hatua ya pili ya usaili kwa vitendo katika kituo alichochaguliwa. Waombaji wawe tayari kujigharamia nauli, malazi na chakula wakati wa usaili kwa vitendo vituoni ndani ya siku saba.
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **07 Septemba, 2022.**
7. Kwa maelezo zaidi wasiliana kupitia namba zifuatazo:-

LITA: 0625 874 298 au 0742 762 364; au
TALIRI: 0763 546 165 au 0785 325 847

IMETOLEWA NA KATIBU MKUU (SEKTA YA MIFUGO)